Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

25/= Ksh

Volume 5, Issue 5

25th Muharram 1432

31st December, 2010

Yaliyomo

Tabia (Adabu) Njema Za Ki-Islamu 1 - 4

Kisa Cha Kukosolewa 'Umar 4

Tabia (Adabu) Njema Za Ki Islamu

Mtayarishi: Al-Ustadh Mahmoud Salaamah Al-Muhri (Al-Isaalah Vol 35-37)

UMUHIMU WA UTEKELEZAJI AHADI NA MIKATABA.

Hakika ya tabia ya utekelezaji wa ahadi na mikataba ni miongoni mwa tabia tukufu (bora). Haiwi tabia hii ni yenye kuenea (na kusambaa) katika umma miongoni mwa umma wowote au katika mijtama' miongoni mwa mujtama' isipokuwa huwa umma ule au mujtama' ule ni wenye kuwa na nguvu, ushikamano na kuongozwa na amani na utulivu na kusaidiana, kuhurumiana nyoyo zao kuwa pamoja na kupendana ukawa ni mujtama' ambao wenye kuheshimika na kupata hadhi mbele ya mujtama' nyenginezo. Na wala haitakuwa ni yenye kukosekana tabia katika ummah au mujtama' miongoni mwa mujtama' za watu isipokuwa mujtama' kama ule huwa ni mujtama' ambao uliogawanyika na kuingiwa na udhaifu ukiongozwa na khofu na kutopatikana utulivu, kubughudhiana, kijipendelea kila mtu nafsi yake, vifundo, hasad, utesi , na kukatana ukawa ni mujtama' ambao ni dhalili (mnyonge) usokuwa na thamani mbele ya mujtama' nyenginezo. Ilipokuwa tabia hii umuhimu wake ni huu ikawa ni lazima kwa kila muislamu kisimama mbele ya tabia hii kwa kuitekeleza na kujipamba nayo ili apate kufanya lenye kumridhisha Mola wake afuzu kwa kupata radhi zake Allaah (سبحانه وتعالى) na kusalimika kutokamana na hasira zake na adhabu yake kali. Kwa ajili ya kutaka kutoa nasaha zangu kwa ndugu zangu waislamu nimejitahidi kukusanya risala hii ndogo yenye faida kubwa na manufaa makubwa katika mlango wa kufundishana. Amesema Allaah **"Na yatoe mawaidha hapana shaka mawaidha yawafaa wenyekuamini."** [Surat adh-Dhaariyaat: 55). Na kuwa ni ukumbusho wenye kumkumbusha: **"Yule ambaye mwenye kutulia katika kusikiliza na ilhali yeye mwenyewe yupo hapo."** [Surat Qaaf: 37). Kwa kumuomba Allaah Sw awanufaishe kwa haya, ndugu zangu waisilamu, na ayafanye kwangu mimi ni khazina (itakayonifaa mimi kesho Akhera) na kuokoka siku ya malipo (siku ambayo hayatomfaa mtu mali yake wala wanawe isipokuwa yule atakaekuja mbele yake Yeye na moyo (ulosalimika) na shirk na bid'ah. Na nimeyagawanya maudhui haya kwa njia, nukta au vidokezo.

NUKTA YA KWANZA:

[MAANA YA AHADI]: Maana ya ahdi imekuja kutoka katika Qaamus (kubwa miongoni mwa Qaamus za lugha ya kiarabu) *Lisaanul Arab* Vol. 3/311. Tamko la ahaadi ni kila ahadi aliyoekewa Allaah (na mwana-adamu) kuitekeleza. Na kila mapatano (ya mikataba) kati ya mja na mwenzake (miongoni mwao), huwa hiyo ni ahadi. Hii ndiyo maana ya tamko la ahadi kilugha. Ama katika misingi ya kisheriya (maana ya utekelezaji ahadi na mikataba) ni kule kutimiza na kutekeleza ahadi zote na mikataba yaliyopo baina ya mja na Mola wake. Na kati ya mja na waja wenzake katika (ahadi zile) alizozihalalisha Allaah (سبحانه وتعالى) kutekelezwa na kuzikubali.

NUKTA YA PILI:

[**HUKMU YA UTEKELEZAJI WA AHADI NA MIKATABA**]: Zimekuja dalili (nusoos) ndani ya Qur'aan Tukufu na Sunnah iliyotakasika juu ya amri ya kujifungamanisha na tabia hii njema. Asema Allaah (سبحانه وتعالى) **"Enyi mulioamni, zitekelezeni ahadi, mmehalalishiwa kwenu wanyama (Ngamia, Ng'ombe, Mbuzi na Kondoo baada ya kuwachinja kula nyama zao) ila walioharamishwa kwenu pasi na kuhalalisha kuwinda na ilhali mwafanya Ihraam. Hapana shaka Allaah yuahukumu akitakacho."** [Surat al-Maaidah Aya 1].

Na akasema tena Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na zitekelezeni ahadi. Hapana shaka ahadi ni zenye kuulizwa."** [Surat al-Israa' Aya 34].

Akasema tena Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na kwa ahadi ya Allaah, itekelezeni"** [Surat al-An'aam 152]

Na akasema Allaah: **"Na itekelezeni ahadi ya Allaah wakati mnapotoa ahadi na wala musizivunje ahadi zenu baada ya kuzithibitisha (mulizozichukuwa baada ya kula yamini), na hakika mumemfanya Allaah kuwa ni shahidi yenu."** [Surat an-Nahl 91] Amesema Mtume (صلى الله عليه

وسلم**):** *"Itekeleze amana kwa yule aliyekuamini (akakupa)na wala usimfanyie khiyana mwenye kukufanyia khiyana* [Swaheeh Sunan at-Tirmidhee].
Akasema Mtume **(**صلى الله عليه وسلم**):** *"Nendeni vitani (mukapigane) wala musifanye khiyana (katika mali ya ngawira – nyara-wala musivunje ahadi)*. [Muslim]
Hizi ni dalili (nusoos) kutoka ndani ya Qur'aan na Sunnah zenye kuamrisha juu ya kujifungamanisha na tabia hii tukufu na amri ikija juu ya jambo huwa yamaanisha ulazima (faradhi) wa kufanywa jambo lile isipokuwa patakapotokea kigeuzi chenye kubadilisha uwajibu ule kutoka katika hukumu ya faradhi ile na hapa hakuna kigeuzi chenye kugeuza kwahiyo hukmu ya uwaajib iko palepale kama ilivyo Qaa'ida (msingi) miongoni mwa Qaaida za Usool al-Fiqh, bali dalili zilizokuja za kukokoteza hilo na kuhimiza hilo.

NUKTA YA TATU:

[QAULI (MANENO) ZA WANAVYUONI JUU YA UTEKELEZAJI WA AHADI]

Asema Imaam Ibn Katheer **(**رحمه الله**):** Katika neno lake Allaah **(**سبحانه وتعالى**): "Na zitekelezeni ahadi za Allaah wakati mnapotoa ahadi."** [Surat an-Nahl: 91]
Asema **(**رحمه الله**):** "Haya ni miongoni mwa yale Allaah alotuamrisha, nayo ni kutekeleza ahadi na mikataba na kuhifadhi viapo." [3/643]
Asema al-Imaam Qurtubee katika neno lake Allaah: **"Enyi mulioamni, zitekelezeni ahadi."** [Surat al-Maaidah Aya 1], 'Aya hii imekusanya ndani yake hukmu tano; La kwanza amri ya kutekeleza ahadi." [Tafseer al-Qurtubee 3/4]. Amesema al-Imaam an-Nawawee katika neno lake Mtume **(**صلى الله عليه وسلم**):** *"Nendeni kapiganeni, wala musifanye khiyana katika mali ya ngawira, wala musivunje ahadi*." [Sherhe ya Swaheeh Muslim]. Akasema na katika hadeeth hii: "...muna faida walizoafikiyana nazo wanavyuoni nayo mojawapo ni uharamu wa kuvunja ahadi." Asema Sheikh Saalih al-Fawzaan **(**حفظه الله**):** "...na kuvunja ahadi ni haramu hata kama ahadi atakuwa mtu ameekeana na makafiri. Hakika ameamrisha Allaah kutekeleza ahadi zao watakapozisimamisha na wala wasiwe ni wenye kuvunja chochote katika ahadi hizo." [khutabul minbariyyah 1/197].
Dalili hizi za Qur'aan na Sunnah na kauli za baadhi ya watu wa 'ilmu zatuonyesha uwajibu (lazima)wa utekelezaji wa ahadi

NUKTA YA NNE:

[NI TABIA ZA MITUME, WATU WEMA NA WAUMINI]

Allaah **(**سبحانه وتعالى**)** asema: **"Na mtaje katika Qur'aan, Isma'eel; hapana shaka alikuwa ni mkweli wa waadi na alikuwa ni Mtume; Nabii."** [Surat Maryam: 54]
Asema Ibn Katheer **(**رحمه الله**):** "Hii ni sifa kutoka kwa Allaah, kumsifu Isma'eel Bin Ibraahim (kipenzi) **(**عليهم السلام**)** (ambayo, yeye Isma'eel ni baba wa waarabu wa Hijaaz wote, yakwamba yeye alikuwa ni mkweli wa ahadi. Asema mwanachuoni (Ibn Jareer) hakutoa ahadi yoyote kwa Mola wake isipokuwa aliitekeleza." [3/139].
Akasema Allaah **(**سبحانه وتعالى**): "Na Ibraahim alotimiza ahadi ya Allaah."** [Surat an-Najm: 37].
Akasema Allaah **(**سبحانه وتعالى**): "Na ambao wao kwa amana zao na ahadi zao ni wenye kuzitunga (wazitekeleza)."** [Surat al-Mu'minoon: 8].
Akasema Allaah **(**سبحانه وتعالى**): "Na ambao huitimiza ahadi ya Allaah na wala hawavundi ahadi."** [Surat ar-Ra'd: 20].
Asema al- Qurtubee **(**رحمه الله**):** kuihusu aya hii: "Hii ni swifa ya wenye akili (yaani) Hakika wenye kuyakumbuka maneno yake ni wale wenye akili. (yaani wenye kutekeleza ahadi. Na tamko la ahadi ni (*ismu jinsi*) yaani ni jina lililokusanya ahadi zote za Allaah, nazo ni amri zake na makatazo yake ambayo alouswiya kwayo waja wake. Na vilevile yaingia katika matamko haya aina zote za faradhi (yale mambo ya wajibu) na kujiepusha na maaswiya yote." [al-Qurtubee 9/265]. Kutaja mifano ya mienendo ya baadhi ya Manabii katika kuzitekeleza kwao ahadi zao ni huyu Mtume wetu **(**صلى الله عليه وسلم**)** (ambae alokuwa tabia yake ni Qur'aan. Hakika amemsifu Allaah aliposema: **"Na hakika yako wewe uko juu ya tabia njema."** [Surat alQalam: 4].
Akiwatekelezea maadui zake ahadi zao katika hali nzito (za mapigano).
Amepokea al- Imaam Muslim kutoka kwa swahaba Hudhaifa Ibnul Yamani **(**رضي الله عنه**)** "Hakuna kilichonizuiya mimi nisishuhudie vita vya Badri isipokuwa mimi nilitoka na babangu (Husaylun) wakatushika Mushrikina (makafiri) wakatuuliza, "Nyinyi mwaelekea Madina kwa Muhammad?" tukawajibu; "Sisi hatwendi kwake ila twenda Madina tu." Basi wakachukuwa kwetu sisi ahadi (kwa Allaah) ya kiapo kuwa WALLAHI tutakwenda Madina, wala hatutopigana na yeye kumsaidia. Tukaja Madina kwa Mtume **(**صلى الله عليه وسلم**)** na tukampa khabari akasema kutwambia, "Nendeni na muitekeleze ahadi muloekeana nao na sisi twamtegemea Allaah juu yao." [*Muslim, al-Haakim, Ahmad; na tizama Silsilat as-Swaheehah 5/224*].
Na katika utekelezaji wake wa ahadi na wake zake (hata baada ya kufa mmoja wao) ni hadeeth aloipokea at-Tirmidhee kutoka kwa nana 'Aaisha asema: "Sikuwahi kumfanyia wivu yoyote katika wake za Mtume **(**صلى الله عليه وسلم**)** kama nilivyomfanyia wivu bibi Khadeejah na mimi sikumpata bibi Khadeejah na si jengine lililonipelekea kufanya hilo) isipokuwa ni kwa sababu ya Mtume **(**صلى الله عليه وسلم**)** alikuwa akimtaja mara nyingi sana." Na alikuwa Mtume **(**صلى الله عليه وسلم**)** akichinja mbuzi na akizunguka kuwagawanyia marafiki wa bibi Khadeejah **(**رضي الله عنها**)** [Swaheeh Sunan at-Tirmidhee 2/196]. Nikasema na kwa nini isiwe hivyo. Naye ni yule alomwambia bibi 'Aaisha **(**رضي الله عنها**)** siku alipokuwa kwake bibi mmoja mtu mzima. Akamuuliza Mtume, "wewe ni

(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)

nani?" akajibu yule bibi, "Mimi ni Juthaama (maana yake tamko hili ni mtu pite asokuwa na maana wala tabia; mvivu) wa kabila la Muzayna. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamjibu, "Wewe ni Hassaana wa kabila la Muzayna (yaani kumbadilisha jina lake la kwanza lililokuwa na maana mbaya na kumpa jina zuri). Akaendelea Mtume (صلى الله عليه وسلم) kumwambia, "Vipi hali zenu, mulikuwaje hali zenu baada yetu sisi?" (yaani baada ya kuondoka bibi Khadeejah (رضي الله عنها) akajibu yule bibi, "Hali zetu ni nzuri ewe Mtume wa Allaah." Alipotoka yule bibi 'Aaisha alisema kumwambia Mtume, "Ewe Mtume wa Allaah, mbona umempokea bibi huyu kwa mapokezi haya ya kumuuliza sana hali zake?" Mtume(صلى الله عليه وسلم) akamjibu, "Huyu bibi alikuwa akija kwetu katika zama za bibi Khadeejah (رضي الله عنها) na hakika ya kuweka uzuri wa ahadi ni katika Imani [Ssilsilatu as-Swaheeha No. 2161]. Na yeye (صلى الله عليه وسلم) ndiye alosema, "*Hakika yangu mimi si mwenye kuwa na sifa ya uvunjaji wa ahadi.*" [Silsilatu as-Swaheeha 2/323; Subul as-Salaam 4/65]. Na kisa cha pili katika visa vya Manabii (عليهم السلام) ni kisa cha Mtume Musa (عليه السلام) Siku alipotoka Misri baada ya kumuuwa Mqibty akawa yuamkimbia Fir'aun na Jeshi lake wasije wakamshika. Alipofika Madyan na kuwasaidia wale wanawake wawili kuwatekea maji, akaketi chini ya kivuli cha mti kujipumzisha na machofu ya safari, alimjilia mmojawapo wa wanawake wale wawili akamwambia kuwa babake amwita ili kwenda kumlipa kwa wema ule alowafanyia mabinti zake. Kama alivyotaja Mola wetu katika Kitabu chake, **"Na alimjia Musa mmoja katika wanawake wawili akitembea kwa miguu akiwa mwenye haya. Alisema , "Hapana shaka babangu yuakuita akulipe malipo ya kutunyweshea wanyama wetu. Basi alipomjia Musa, kwa baba (ya wanawake wawili na kumzungumzia khabari yake) alisema baba, "Usiogope , umeokoka na Fir'aun na watu wake". Alisema mmoja wao (wa wale wasichana), "Ewe babangu muajiri kazi, hapana shaka bora wa utakaomuajiri kazi ni mwenye nguvu, Muaminifu. Alisema (baba) hapana shaka mimi nataka kukuoza mmoja katika watoto wangu wawili hawa kwa sharti ya ufanye kazi ya uchungaji kwa muda wa miaka minane. Na ukitimiza miaka kumi basi itakuwa ni Ihsani yako, na wala sitaki kukulazimisha. Utanikuta Allaah akipenda ni miongoni mwa watu wema. Alisema Musa hayo (tuliyosikizana) baina yangu na wewe muda wowote katika muda miwili (miaka Minane au Kumi) nitakayoifanyia kazi nisidhulumiwe na Allaah mnayoyasema ni mwenye kushuhudia."** [Surat al-Qasas 25-28].

[KUTAJA MIFANO YA UTEKELEZAJI WA AHADI KATIKA QARNE BORA ZA MASWAHABA]

KISA CHA ANAS BIN NADHAR (رضي الله عنه)

Alikuwa huyu Anas Bin Nadhar (رضي الله عنه) hakuhuduriya katika via vya Badr na hakuna yoyote aliyemlaumu na Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwaamrisha watoke kwa kuwalazimisha. Isipokuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alitoka na baadhi ya Maswahaba kwenda kuuzuiya msafara wa Maquraysh ndipo vikazuka vita vya Badr. Ushindi ukawa ni wa Waislamu. Akasikiya utungu swahaba huyu na majuto kwa kutohudhuriya vita vya kwanza vya ki-Islamu (Jihaad). Akampa Anas ahadi Mola wake atakapomja'aliya Allaah kuvishuhudiya vita atakavyofanya. Anas akashiriki katika vita vya Uhud na akafa Shaheed akawa ni mwenye kuitekeleza ahadi ile.

[KUVUNJA AHADI NA KUTOITEKELEZA PASI NA UDHURU WA KISHERIYA NI KATIKA ALAMA ZA WANAFIKI]

Allaah (سبحانه وتعالى) asema: **"Jee na Kila wanapoahidi ahadi yoyote huivunda kundi miongoni mwao, basi wengi wao hawaamini."** [al-Baqarah: 100].

Akasema tena, **"Hapana shaka viumbe vibaya mbele ya Allaah ni wale waliokufuru, basi wao hawaamini. Ambao ulifanya ahadi nao (kwamba wasiwasaidie washirikina) kisha wanavunja ahadi yao kila mara na ilhali wao hawamuogopi Allaah."** [al-Anfaal: *55 -56*].

Akasema Allaah tena. **"Na miongoni (mwa wanafiki) kuna waliomuahidi Allaah. Wallaahi akitupa Allaah miongoni mwa vipawa vyake wallaahi tutatoa tutatoa sadaka na wallaahi tutakuwa tutakuwa katika watu wema. Na alipowapa (Allaah) miongoni mwa fadhila zake walizifanyia ubakhili walivunja ahadi na waliwacha kumtwi'i Allaah, basi Allaah aliwatia ndani ya nyoyo zao unafiki mpaka siku ya kukutana naye kwa sababu walivunja ahadi yao na Allaah. Na kwa waliyokuwa wakiyasema ya uongo."** [Surat at-Tawbah: *75-77*].

Asema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "*Alama za mtu mnafiki ni tatu; akizungumza husema urongo; akitoa ahadi huikhalifu na akiaminiwa hufanya khiyana.*" [al-Bukhaari].

[MIFANO YA UVUNJAJI WA AHADI ZA MAKAFIRI NA WANAFIKI PASI NA UDHURU WA KISHERIYA]

KABILA LA BANU QURAIDHA

Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliekeana nao mkataba alipokuja Madina yakuwa wasimsaidie adui yoyote wa Waislamu na wala Waislamu wasimsaidie adui yoyote wao (banu Quraidha), lakini pamoja na hayo wao kama kawaida yao wakavunja ahadi katika vita vya Ahzaab wakawasaidia makafiri na baada ya vita hivyo (vya Ahzaab) akawazingira Mtume siku kumi na tano. Akamtuma Mtume (صلى الله عليه وسلم) Lubaabah Ibnul Mundhir, wakakubali kuhukumiwa na Sa'ad Bin Mu'aadh. Akatoa hukmu swahaba huyu kuwa kila

mwanamume alobaleghe akatwe kichwa na wanawake wao na Mali zao ziwe ngawira kwa Waislamu. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: *"Hakika amehukumu leo juu yao (banu Quraidha) kwa hukmu ambayo ilokuwa ishapitishwa kwenye mbingu saba."* [Amepokea an-Nasaa'i na Ibnu Sa'ad katika Twabaqaat na Silsilatus swaheeha]. Na kisa cha pote la wanafiki lililomuahidi Mola wao na lisitekeleze. [Suraat at-Tawbah: 75-76].Asema al-Haafidh Ibnu Katheer katika aya hizi: "Asema Allaah, 'na miongoni mwa wanafiki wako walompa ahadi Mola wao yakuwa atakapowakwasisha (kuwapa uwezo) katika fadhla zake basi watatoa sadaka katika mali zao na watakuwa miongoni mwa watu wema. Na wala wasitekeleze waliyoyasema. Allaah akapiga muhuri wa unafiki nyoyoni mwao mpaka siku ya kukutana nao siku ya Kiyama.'" [Tafseer Ibnu Katheer 2/411]

[KATIKA KUMTETEA SWAHABA THA'LABA KUTOKANA NA ALIYOZULIWA NAYO]

Baadhi ya wanavyuoni wa Tafseer katika munaasaba wa aya hii tuliyoitaja (Suraat at-Tawbah 75-76) sasa hivi yakuwa iliteremka kwa Tha'laba Bin Haatib, Swahaba Mtukufu Siyo kweli (Si kisa cha ukweli). Amesema Imaam al-Qurtubee (رحمه الله) [134-8/133]: "Na hakika wametaja baadhi ya Mufassireen yakwamba hakika ya sababu ya kuteremka aya hizi iliteremka kwa Tha'laba Bin Haatib. Na Tah'laba ni katika Maswahaba waliohudhuriya vita vya Badr. Na ni miongoni mwa watu ambao Allaah na Mtume wake waloshuhudia juu ya kuamini kwake ,... kilichopokewa juu ya kisa hiki si swaheeh."Asema al-Haafidh katika Fat-hul-Baari 3/266 katika hadeeth ilokuja (juu ya kisa hiki cha Tha'laba) "Iakini ni hadeeth Dha'eef, haitolewi Hujja." Na ametunga ndugu yangu mpendwa, Sheikh Salim al-Hilaali kitabu kamili katika kukirudi kisa hiki akikiita (Ash-Shihaabuth-Thaaqib fee Dhabbi 'Anys-Swahaabiyya Haatib) nacho ni kitabu kizuri, hakika amekiandika vizuri na chenye faida. Allaah amjazi kheri anaetaka kujua zaidi (juu ya kisa hiki) na arudi katika kitabu hiki.

[ENDELEA KATIKA MAKALA YAJAYO]

KISA CHA KUKOSOLEWA 'UMAR NA MWANAMKE

Kuna kisa kilichonukuliwa tangu zama za 'Umar Ibn al-Khattaab kwa madai yakwamba alikusudia kujaribu kuweka kiwango maalum cha mahari anayolipwa mwanamke pindi anapo-olewa. Kisa chaeleza yakwamba baada ya 'Umar Ibn al-Khattaab kulingania mwito huwo akiwa juu ya minbar na kubainisha yakwamba iwapo mtu atatowa zaidi ya kiwango alichotowa Mtume (صلى الله عليه وسلم) atakiweka kiwango hicho cha ziyada kwenye Hazina za Umma. Akamjilia mwanamke kutoka katika kabila la Quraysh na akamwambia, "Ewe kiongozi wa Waumini, Kitabu cha Allaah kina haki zaidi kufuatwa au maneno yako?" Akasema, "Kitabu cha Allaah." Basi yule mwanamke akamwambia, "Wewe umewaharamishiya watu wasitoe kiwango cha ziyada katika mahari, haliyakuwa Allaah (سبحانه وتعالى) amesema katika kitabu chake Kitukufu: **"Na hali mmoja wao mmempa mrundi wa mali, basi msichukuwe chochote."** [an-Nisaa' 4:20]. Kisha 'Umar akasema mara mbili au tatu, "Kila mmoja ana ufahamu mzuri kuliko 'Umar." [baadhi za riwaya zaeleza: "Huyu mwanamke amepata na 'Umar amekosea." Nukta za chini]. Kisha akapanda tena juu ya minbar na akasema "Enyi watu! Nilikuwa nikiwakataza musizidishe katika mahari ya wanawake. Kwa hakika mtu anaruhusiwa kufanya aonavyo ni sawa na mali yake." Kisa hiki kimesimuliwa na al-Baihaqee katika Sunan al-Kubra na 'Abdul-Razzaq katika al-Musannaf. Silsila hizo zao, al-Baihaqee na 'Abdul-Razzaq ni dha'eef. Kwa hakika, al-Baihaqee ameeleza yakwamba silsila aliyoinukuu yeye imekatika. [Abu-Bakr al-Baihaqee, Sunan al-Kubra, Beirut, Dar al-Fikr, Vol 7, Uk. 233].

Kwa hakika, yaonekana kama kwamba Imaam al-Baihaqee ameipendekeza riwaya nyengine kutoka kwa 'Umar aliyoipokea punde tu baada ya riwaya hiyo ya hapo juu. Katika riwaya hiyo, yasema yakwamba 'Umar amesema alikuwa amekusudia kuweka kiwango maalum kwenye mahari ya wanawake mpaka alipoisoma aya, **"Mrundi wa mali."** Katika kuizungumzia riwaya hii, al-Baihaqee amesema, "Ni silsila nzuri ya upokezi." [Nukta ya chini: Maana ya Mursal ni kukatika kiungo baina ya 'Umar na aliyeipokea kutoka kwake].

Imaam al-Albaani ametaja yakwamba licha ya udhaifu wa silsila za upokezi za al-Baihaqee na 'Abdul-Razzaq kwa sababu ya kukatika kwake, bali ndani yake vilevile kuna wapokezi walio dhaifu waliozidisha udhaifu wa silsila zake. Kwahiyo, hatimaye ameihukumu riwaya hii itokayo kwa 'Umar Ibn al-Khattaab kuwa ni dhaifu bila ya shaka yoyote. [Nukta ya chini: *Muhammad Naasir ud-Deen al-Albaani; Irwaa ul-Ghaleel Fee Takhreej ahaadeeth Manar as-Sabeel;* Beirut, Al-Maktab al-Islaami, 1979, Vol. 6, Uk. 347].

Hapana shaka, imethubutu katika hadeeth swaheeh iliyopokewa na Abu Daawud, an-Nasaa'ee, at-Tirmidhee na wengineo yakwamba kwa hakika 'Umar Ibn al-Khattaab aliwausiya watu wasifanye israfu inapokuja kuhusu mas'ala ya mahari ya wanawake.

Kwa kweli, tukio hilo la hapo juu tangu kwenye zama za 'Umar Ibn al-Khattaab, linanukuliwa na watu wengi siku hizi katika kuthibitisha yakwamba wanawake walikuwa wakijitokeza waziwazi kwenye ulingo wa kisiyasa na harakati nyenginezo katika zama za Maswahaba. Walikuwa na ushawishi mkubwa kwenye jamii, na chembelecho mzungumzaji mmoja leo anavoiita, "... alikuwepo kwenye kongamano. (!) lililofanyika msikitini wakati huwo." Wanazidi kutoka hapo kuwashawishi wanawake wachukuwe hatamu zenye msukumo wa nguvu katika jamii badala ya kutosheka na kubaki nyumbani na kuwa ni wake na wazazi watiifu tu. Wanasema yakwamba huu haukuwa ni mwenendo katika zama za Maswahaba kama kisa hiki wakati wa 'Umar kinavyo ashiriya waziwazi. Ni wazi yakwamba, maadamu twataka kutumia kisa kama hicho kuwa ni dalili, ni lazima kwanza mtu athibitishe uswaheeh wa riwaya hiyo. Hili haliwezekani katika mas'ala haya na kwahivyo, kisa hiki hakiwezi kutumika kuwa ni dalili. **Na Allaah ndiye Mjuzi Zaidi.**